JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA UTALII

**WIZARA YA UTALII, MALIASILI NA MAZINGIRA,**
**DAR ES SALAAM**

**Mwanachama wa WTO**

# YALIYOMO

| | Ukurasa |
|---|---|
| Tamko Maalum la Arusha | v |
| Utangulizi | 1 |
| Maana na tafsiri ya Mtalii | 3 |
| Vivutio vya Utalii Tanzania | 4 |
| Madhumuni ya jumla ya Sera | 7 |
| Ufafanuzi wa utekelezaji wa Sera | 8 |
| Uimarishaji wa huduma nyingine za Kitalii | 19 |
| Mengineyo | 20 |
| Mwisho | 20 |
| **Viambatisho:** | |
| (a) Tamko Rasmi la Halmashauri Kuu ya Taifa kuhusu Utalii | 21 |
| (b) Vivutio kwa Wawekezaji Raslimali Tanzania | 23 |
| (c) Ramani ya Vivutio vya Utalii Tanzania | 29 |

© Haki ya kunakili imehifadhiwa.

*Toleo la kwanza — 1991*

**Kimetolewa na Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira**
**na kupigwa chapa na**
**Kitengo cha Uchapaji cha Shirika la Posta na Simu Tanzania— Dar es Salaam**


## TAMKO MAALUM LA ARUSHA

Kudumu kwa maisha ya wanyama wa porini ni jambo linalotuhusu sana sisi wote katika Bara la Afrika. Viumbe hawa si maajabu na fahari ya nchi yetu tu bali pia ni sehemu mojawapo ya uchumi wetu wa asili na starehe ya maisha yetu ya kesho.

Katika kuchukua dhamana na ulinzi wa wanyama wa porini twathibitisha kwamba tutafanya kila tuwezavyo katika mamlaka yetu kuhakikisha kwamba watoto wetu wa kesho kutwa wanaweza kufaidi utajiri na uhondo wa urithi huu.

Utunzaji wa wanyamapori na misitu yake unahitaji ujuzi maalum, watu waliofundishwa kadhalika na fedha, na kwa hivyo twataraji mataifa ya kigeni yatashirikiana nasi katika kazi hii muhimu ambayo kutokufaulu kwake, licha ya kuwa ni madhara katika Bara zima la Afrika yatakuwa ni madhara katika ulimwengu wote.

Julius K. Nyerere
7.9.1961


Nimeponzwa
na
pembe
yangu

## UTANGULIZI

1. Tanzania, mojawapo katika nchi kubwa barani Afrika, iko katika Ukanda wa Pwani ya Mashariki ya Afrika, kati ya Latitudi 1 na 11 kusini mwa Ikweta. Eneo la Tanzania ni kilomita za mraba 945,000; ambazo ni sawa na eneo la nchi za Denmark, Ufaransa, Uholanzi, Jamhuri ya Ireland na Uingereza kwa pamoja. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajumuisha sehemu iliyokuwa inajulikana kama Tanganyika na Visiwa vya Zanzibar.

2. Sensa iliyofanyika nchini mwaka 1988 inaonyesha kuwa Tanzania inao wakazi milioni 23.17, na idadi hii huongezeka kwa asilimia 2.8 kwa mwaka. Kati ya wakazi hawa, milioni 22.53 wako Tanzania Bara na 640,000 wako Visiwani.


3. Tanzania inapakana na Kenya na Uganda upande wa Kaskazini; Rwanda, Burundi na Zaire upande wa Magharibi; Zambia, Malawi na Msumbiji upande wa Kusini na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Njia kuu za usafiri ni barabara, reli, anga na meli. Tanzania inazo bandari kuu nne - Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara na viwanja vya ndege vya kimataifa vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar. Vipo viwanja vingine vingi vilivyotapakaa mikoani. Mawasiliano ya njia za simu na nchi nyingine yameimarishwa.

4. Serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika uimarishaji wa huduma za jamii kama vile elimu, afya na huduma nyingine kwa jamii.

5. Tanzania ni nchi inayoendelea ambayo bado uchumi wake ni duni. Mapato ya nchi hutegemea uzalishaji wa vijijini na kilimo ndicho uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa. Kilimo huchangia asilimia 50 ya pato la taifa na asilimia 80 ya watanzania wanajihusisha na kilimo.

6. Serikali imechukua hatua kadhaa za kuimarisha uchumi.

# Ni Tembo tu mwenye haki ya kuvaa vipusa



go yaliyokusudiwa, kuna haja ya kuongeza ushirikiano kati ya pande zote zinazohusika na uendelezaji wa utalii nchini Tanzania. Sera hii ni hatua mojawapo muhimu ya kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa na nafasi muhimu katika ramani ya utalii ulimwenguni katika karne ya 21. Vilevile inaiongezea nguvu Sera ya Uwekezaji Raslimali ambayo ilitolewa mwaka 1990 ili kuhimiza na kuhuisha uwekezaji wa raslimali nchini.

**Maana na Tafsiri ya Mtalii:**

11. Kutokana na tafsiri za kimataifa na ile ya Shirika la Utalii la Dunia, mtalii ni mtu yeyote yule anayesafiri nje ya maskani yake ya kawaida na kwenda sehemu nyingine na kukaa huko kwa zaidi ya saa 24 kwa madhumuni yaliyo tofauti. Safari hizo zinaweza kuwa za kibiashara, kuhudhuria mikutano au likizo. Utalii unaweza kuwa wa ndani ya nchi ambao hufanywa na wananchi. Tofauti kubwa kati ya utalii wa wananchi na utalii wa kimataifa ni kwamba mtalii wa kimataifa hulipia gharama zake katika fedha za kigeni na mtalii mwananchi hulipia gharama zake katika fedha za nchi yake.

12. Zipo shughuli mbalimbali ambazo mtalii huweza kuzifanya katika sehemu anazotembelea. Shughuli hizi hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine kulingana na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya nchi inayohusika na mahitaji ya kila mtalii. Hata hivyo baadhi ya shughuli ambazo mtalii huzifanya ni kutembelea mbuga za wanyama na kuwinda, kupiga picha, kuchunguza mimea na wanyama, kuvua, kuogelea na kufanya michezo mingine ya majini, kuona mambo ya kihistoria kama magofu, makaburi ya kale na kadhalika, kupanda milima, kuhudhuria mikutano, kujipumzisha, shughuli za biashara na kutembelea ndugu, jamaa na marafiki baada ya shughuli za uzalishaji.

Baadhi ya hatua muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka mkakati wa kuongeza pato la fedha za kigeni kwa kuhimiza uuzaji nje wa mazao yasiyo asilia pamoja na mboga na matunda na pia kulegeza masharti ya biashara.

7. Ingawaje Tanzania inazo raslimali kubwa na vivutio vingi vya utalii, bado hatua ambazo hadi sasa zimeshachukuliwa kuimarisha sekta hii hazijaweza kuitumia kikamilifu hazina ya vivutio hivi kwa njia ya Utalii. Sera hii ya Utalii inalenga katika kuikuza na kuiimarisha sekta ya Utalii ili iweze kuchangia zaidi katika mapato ya taifa kwa ujumla, iongeze ajira ya wananchi na ichangie katika kupanua uzalishaji bidhaa na utoaji wa huduma mbalimbali.

8. Tanzania ilijipatia jumla ya dola za kimarekani milioni 18 mwaka 1980 na dola milioni 65 mwaka 1990 kutokana na utalii. Lakini utajiri wa maliasili na vivutio vya utalii nchini vingepaswa kuifanya nchi hii kuingiza fedha zaidi za kigeni. Inategemewa kwamba mapato kutokana na utalii yatafikia dola za kimarekani milioni 500 ifikapo mwaka 1995.

9. Utalii hivi sasa ni biashara ambayo inachukua nafasi ya pili katika kuipatia Tanzania fedha za kigeni. Lengo la Sera hii ni kuuwezesha utalii kuingiza fedha zaidi za kigeni ili hata kuufanya utalii uchukue nafasi ya kwanza katika uingizaji wa fedha za kigeni. Wakati huo huo, jitihada zitafanyika kuhakikisha kwamba vivutio vya utalii ambavyo ni urithi wenye thamani kubwa kwa dunia nzima na ambavyo Tanzania imethaminiwa kuvitunza, vinaendelea kuwa katika hali nzuri.

10. Mwelekeo wa Sera hii ni kuimarisha huduma za utalii nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa raslimali wa ndani na nje na kuvitangaza vivutio vya utalii nje ya nchi. Sera inaainisha majukumu ya Serikali, Mashirika ya Umma, Mashirika ya Kimataifa na watu binafsi katika kuendeleza utalii. Sera hii inatambua kwamba katika kuyafikia malen-

volkano hiyo kilianguka na kufanya shimo kubwa lenye kina cha mita 610 na urefu wa kilomita 20. Eneo lote la mbuga hii ni kilometa za mraba 311.

### 13.2.3 Sehemu ya Olduvai:

Olduvai inajulikana kama mahali ambapo mtu wa kale aliishi. Mabaki ya mtu wa kale aliyejulikana kama "nutcracker man" yaligunduliwa mwaka 1959 na mchunguzi maarufu wa mambo ya kale, Dr. Leakey. Miaka 29 baadaye, mwaka 1979, mke wa Dr. Leakey, Mary aligundua mabaki ya mtu wa kale aliyeishi karibu miaka milioni tatu na nusu katika eneo la Laetoli.

### 13.2.4 Hifadhi ya Ziwa Manyara:

Hifadhi hii ina eneo la kilometa za mraba 325 na inasifika kwa kuwa na simba wanaopanda mitini. Pia kuna chemchem ya maji moto (Hot Springs).

### 13.2.5 Hifadhi ya Ruaha

Hifadhi hii inasifika kwa kuwa na ndege na Tembo wengi.

### 13.2.6 Hifadhi ya Selous

Selous ni maskani ya Tembo wengi kuliko sehemu yoyote ile barani Afrika. Vilevile hifadhi hii inalo eneo kubwa kuliko hifadhi zingine za Kiafrika.

## 13.3 Ufuko wa Bahari

Tanzania inao ufuko wa bahari wenye urefu wa kilomita 804 ambao ni mtulivu kwa ajili ya kujipumzisha. Ukanda huu umefunikwa na minazi na ni sehemu nzuri ya kuogelea. Ukanda wa Pwani ya Tanzania unatoa burudani ya aina yake kwa kutoa mandhari ya ajabu na fursa ya kufanya shughuli mbalimbali za kitalii ikiwa ni pamoja na

**Vivutio vya Utalii:**

13. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zenye vivutio vingi vya asili ambavyo ni muhimu katika kukuza na kuendeleza utalii. Baadhi ya vivutio hivi bado havijatumiwa kwa ukamilifu katika kuwavutia watalii wa nje na ndani kuzitembelea sehemu hizo. Baadhi ya vivutio vikuu ni:

**13.1 Mlima Kilimanjaro**

Mlima huu ni mrefu kuliko mingine yote katika bara la Afrika. Una urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari na umezungukwa na msitu mkubwa ambao umejaa mimea ya kila aina. Mlima Kilimanjaro huvutia wapanda milima na wanasayansi mbalimbali ambao hupenda kufanya utafiti juu ya mimea iliyoko kwenye miinuko ya mlima huo.

**13.2 Mbuga za Wanyama**

Tanzania ndiyo nchi ya kwanza duniani yenye utajiri mkubwa wa wanyamapori kwa wingi na kwa kila aina. Wanyama hao wamehifadhiwa na wanaonekana katika mbuga za wanyama ambazo baadhi yake ni:

**13.2.1 Serengeti**

Hifadhi ya Serengeti ambayo inajulikana dunia nzima ni maskani ya wanyama wa aina mbalimbali wapatao milioni nne. Kwa kipindi cha mwaka mzima, wanyama hawa hurandaranda kwenye mbuga hii katika makundi makubwa wakitafuta malisho na maji.

**13.2.2 Ngorongoro**

Hifadhi ya Ngorongoro ni ya kipekee kwa kila hali. Ngorongoro imekwishawahi kuelezewa kama mojawapo kati ya maajabu ya dunia. Miaka ipatayo milioni nane iliyopita, Ngorongoro ilikuwa ni volkano lakini kilele cha

nafasi yake inayostahili duniani katika biashara ya utalii.

## MADHUMUNI NA MALENGO YA JUMLA YA SERA

14. Sera ya Utalii ina madhumuni na malengo ya jumla yafuatayo:

14.1 Kuongeza mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa kwa kukuza na kuimarisha shughuli za kiuchumi zinazoambatana na biashara ya utalii kama kilimo, viwanda, mawasiliano na uchukuzi, mila, desturi, sanaa, utamaduni na kadhalika.

14.2 Kuongeza pato la fedha za kigeni kwa kuongeza idadi ya watalii na siku zao za kukaa nchini na kuchukua hatua zitakazoimarisha ukusanyaji na udhibiti wa fedha za kigeni.

14.3 Kuimarisha na kudumisha vyombo mbalimbali vinavyohusika na biashara ya utalii ili kuanzisha, kupanua na kuimarisha huduma za utalii na kujenga uhusiano na utaratibu wa karibu na vyombo hivi.

14.4 Kuimarisha na kuendeleza mafunzo ya kada mbalimbali katika uendeshaji wa biashara ya utalii katika fani za uendeshaji wa hoteli, huduma, uhandisi, uwakala, uongozi, uokoaji, upishi na kadhalika.

14.5 Kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utalii wa wananchi unaimarishwa na kuendelezwa.

14.6 Kutazama upya sheria zilizopo zinazohusu biashara ya utalii kwa nia ya kuzifanyia marekebisho ili kuimarisha na kuendeleza shughuli za utalii nchini. Aidha, sheria mpya zitatungwa kukidhi haja na mazingira yaliyopo katika kuendeleza utalii nchini.

14.7 Kukuza, kuendeleza na kuimarisha masoko ya utalii ili

uvuvi na michezo ya baharini. Hali ya ukanda wa pwani bado haijachafuliwa na uchafu wa viwandani kama ilivyo katika sehemu nyingine duniani. Hivyo inatoa nafasi nzuri ya kukuza na kuendeleza utalii.

### 13.4 Visiwa vya Zanzibar, Pemba na Mafia

Visiwa vya Zanzibar hasa Pemba ni mashuhuri kwa karafuu. Zanzibar inavyo vivutio vingi vya utalii kama vile majengo ya zamani, barabara nyembamba sehemu ya "Stone Town" na utamaduni, na mila za Watanzania wanaoishi huko.

Kisiwa cha Mafia kinasifika kwa kuwa na sehemu nzuri za kufanya michezo ya majini ikiwa ni pamoja na kupiga mbizi na uvuvi wa kina kirefu.

### 13.5 Magofu ya kale

Tanzania inayo magofu mengi yanayoelezea historia ya nchi hii. Haya ni pamoja na magofu ya Zanzibar, Bagamoyo, Kilwa, Mapango ya Amboni, michoro ya mapangoni sehemu za Kondoa Irangi, na sehemu nyingine. Kumbukumbu hizi zinatoa historia ya maendeleo ya Mtanzania katika nyakati mbalimbali.

### 13.6 Mila, Desturi na Utamaduni wa Watanzania

Watanzania wana mila, desturi na utamaduni wa aina mbali mbali na wana sifa ya ukarimu na umoja. Tanzania ina zaidi ya makabila 120 lakini inayo lugha moja ya Taifa ambayo ni Kiswahili, lugha ambayo inaendelea kukua na kutumiwa na mataifa mengine. Pia yapo makabila mengi yenye sifa kubwa ya kutengeneza vyombo vya mikono kama vile vikapu, mikeka na uchongaji wa vinyago. Ni dhahiri kwamba utajiri mkubwa uliopo nchini bado haujatumiwa kwa ukamilifu ili kuiweka Tanzania katika

15.1.4 Hatua za kuimarisha utoaji huduma nyingine kwa watalii zitaendelezwa.

### 15.2 Kuongeza Fedha za Kigeni

15.2.1 Lengo litakuwa kuongeza fedha za kigeni kwa kuongeza idadi ya watalii kutoka nje na siku zao za kukaa nchini.

15.2.2 Hatua za kuimarisha ukusanyaji wa fedha za kigeni zitachukuliwa kwa kuimarisha sheria za udhibiti wa fedha za kigeni.

15.2.3 Chama na Serikali vitaendelea kuhimiza matumizi ya malighafi za humu humu nchini ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni za kuagizia malighafi hizo kutoka nchi za nje.

15.2.4 Ili kuwahamasisha na kuwavutia watalii wengi, Serikali itaangalia uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kuweka kiwango cha kitalii cha kubadilisha fedha za kigeni (tourist exchange rate) mpango ambao utasimamiwa na benki zetu. Uzoefu wa nchi nyingine katika kuendesha mpango huu utazingatiwa.

### 15.3 Kuimarisha Mafunzo

15.3.1 Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii cha Forodhani kitaimarishwa ili kitoe mafunzo ya hali ya juu na kuweza kukidhi mahitaji ya wataalam mbalimbali wa sekta ya utalii nchini. Hii ni pamoja na kukipatia walimu wa kutosha na wenye sifa na ujuzi unaotakiwa. Mafunzo ya vitendo yataimarishwa.

15.3.2 Ili kuimarisha mafunzo, hatua za kuwapeleka baadhi ya wafanyakazi wa utalii nchi za nje zitachukuliwa, hasa katika maeneo ambako utaalamu huo hauwezi kupatikana hapa nchini.

15.3.3 Mipango ya kubadilishana uzoefu kati ya wataalam wetu

na nchi nyingine itaimarishwa kwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi, semina, warsha, kongamano, mikutano na kubadilishana wataalam.

15.3.4 Ajira ya wafanyakazi wa sekta ya utalii itazingatia uzoefu na utaalam.

15.3.5 Wizara itaandaa mara kwa mara mpango wa mafunzo ya msasa kwa wafanyakazi wanaoshughulikia fani zote za utalii.

15.3.6 Ili kukidhi mahitaji ya wataalam katika sekta ya utalii, mipango itafanywa kujenga chuo kipya cha utalii. Aidha Serikali itahakikisha chuo hicho kinapewa walimu na vifaa vya kutosha.

**15.4 Kuendeleza Utalii wa Wananchi**

Hali ya utalii wa wananchi ni hafifu kutokana na uwezo mdogo wa wananchi wengine kuweza kumudu gharama za utalii katika sehemu za vivutio na kutokuwepo kwa mipango madhubuti ya kuimarisha utalii wa aina hii nchini. Serikali itaandaa mipango mahususi ya utalii wa wananchi kwa sababu kuu mbili:

15.4.1 Kufidia pengo la matumizi ya hoteli na loji zetu wakati wa msimu hafifu.

15.4.2 Kuwapa nafasi wananchi kujifunza na kujionea wenyewe rasilimali kubwa ya Taifa iliyopo kwa kuwapa fursa ya burudani na ya kujipumzisha baada ya kazi nyingi. Kwa kuanzia mkakati wa kuimarisha utalii wa wananchi utalenga kwenye wageni waishio nchini kwa shughuli mbalimbali, wafanyakazi, wakulima na wanafunzi.

15.4.3 Ili kuimarisha utalii wa wananchi, Chama na Jumuiya zake, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na za Vijiji, Mashirika ya Umma, ya Watu Binafsi na Vyama vya Ushirika vitashirikishwa katika kufanikisha mpango

huu. Kwa mfano wafanyakazi wanaweza kujiwekea akiba kutokana na mishahara yao kwa utaratibu maalum utakaowekwa ili hatimaye akiba hiyo iweze kutumiwa na wafanyakazi hao kwa shughuli za utalii. Aidha, waajiri wanaweza kusaidia kufanikisha mpango huu kwa kutoa misaada ya fedha, usafiri na mambo mengineyo. Kwa upande wa wakulima Serikali za vijiji kwa kushirikiana na vyama vya msingi zitashirikishwa kuhakikisha wakulima nao wanapata fursa ya kutembelea sehemu muhimu za utalii nchini. Wizara mara kwa mara itaangalia na kuhakikisha inahuisha bei za utalii kwa nia ya kuzipunguza hasa wakati ambapo watalii kutoka nje si wengi ili kutoa nafasi zaidi kwa wananchi kushiriki katika utalii wa ndani.

### 15.5 Kuimarisha Huduma za Usafiri

Utoaji wa huduma bora kwa watalii hutegemea usafiri ulio mzuri na wenye kuaminika. Sekta hii muhimu imekuwa ikikabiliwa na matatizo kadhaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha za kigeni za kununulia zana, vifaa na vipuri ambavyo ni muhimu katika utoaji wa huduma bora za usafiri. Ili kuhakikisha rasilimali zote za kitalii zinatumika kwa ukamilifu, hatua zifuatazo zitachukuliwa:

#### 15.5.1 Usafiri wa Barabara

15.5.1.1 Jitihada zitafanywa za kuipatia sekta ya utalii magari na vipuri vinavyohitajika katika kukuza utalii nchini kutegemeana na uwezo na hali itakavyokuwa kwa wakati huo.

15.5.1.2 Hatua za kutengeneza na kuimarisha barabara muhimu zilizopo kwenye sehemu za utalii zitachukuliwa. Nguvu za wananchi na sekta ya binafsi zitashirikishwa kusaidia kuimarisha ujenzi wa barabara.

15.5.1.3 Serikali itaendelea na juhudi za kutengeneza barabara

kuu zinazounganisha Kanda za kitalii.

15.5.1.4 Serikali itaangalia uwezekano wa kurekebisha kodi ya mauzo na ushuru kwa zana ziingiazo nchini kwa ajili ya sekta ya utalii na sekta nyinginezo kwa nia ya kuzipunguza ili kuimarisha shughuli za utalii nchini.

### 15.5.2 Usafiri wa Anga

Watalii wengi kutoka nchi za nje hutumia usafiri wa ndege za kimataifa kuingia nchini na pia usafiri wa ndege ndani ya nchi. Usafiri wa ndege ndani ya nchi unakabiliwa na matatizo ya uchache wa ndege, upungufu wa vipuri na wataalam na uwezo mdogo. Ili kukabiliana na hali hii hatua zifuatazo zitachukuliwa:

15.5.2.1 Kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania kwa kulipatia ndege zaidi, vipuri na wataalam ili liweze kutoa huduma bora zaidi ndani na nje ya nchi, na kuliwezesha kusafirisha watalii zaidi waingiao nchini. Lengo litakuwa kuhakikisha kwamba watalii wengi zaidi wanaingia nchini moja kwa moja.

15.5.2.2 Serikali itaangalia uwezekano wa kuanzisha kampuni za ndege za kukodisha (air charter companies) aidha kwa kuanzisha makampuni hayo pekee au kwa kushirikiana na mataifa au makampuni ya binafsi ya ndani na nje kwa mtindo wa ubia.

15.5.2.3 Juhudi za ushirikiano wa karibu zaidi kati ya Tanzania na mashirika mengine ya kimataifa zitachukuliwa. Aidha mpango utafanywa na kutoa motisha kwa mashirika ya ndege yanayoleta watalii wengi nchini.

15.5.2.4 Serikali itachukua hatua za kuimarisha na kupanua viwanja vya ndege mikoani na kuvipatia vifaa na wataalam wa kutosha ili viweze kuhudumia watalii wengi zaidi.

maalum la Arusha lililotolewa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1961 lilieleza kwa undani madhumuni na umuhimu wa kuhifadhi wanyamapori na mazingira yao hapa nchini. Hivyo ili kuendeleza azma hii:

15.6.1 Serikali itaendelea kutunga, kuweka, kurekebisha na kusimamia sheria za hifadhi za wanyamapori ndege na maeneo mengineyo ya kumbukumbu kwa ajili ya manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

15.6.2 Hali ya ujangili na uvuvi haramu unahatarisha maisha ya wanyamapori na samaki walio wengi. Sheria za kupambana na uhalifu huu zitaimarishwa. Vikosi vya kupambana na ujangili na uvuvi haramu vitaimarishwa kwa kuvipatia zana bora za kufanyia kazi na mafunzo.

15.6.3 Sheria za kulinda mazingira katika maeneo ya utalii zitatungwa na kuimarisha zilizopo ili kuhifadhi mazingira kwa kupambana na kuchafuka kwa mazingira ya pwani zetu kutokana na uchafu wa viwanda, tabia ya binadamu kutojali matumizi bora ya maliasili na uhifadhi na uvuvi haramu unaoharibu samaki na matumbawe.

15.6.4 Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine zinazohusika itaendelea kutenga na kusimamia maeneo yanayofaa kwa shughuli za utalii. Ramani za miji na hasa jiji la Dar es Salaam zitaelekeza na kuonyesha waziwazi maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya ujenzi wa hoteli za kitalii ili kuepuka ujenzi holela wa hoteli.

15.6.5 Ukanda wa pwani uliopo utaimarishwa kwa kuendelezwa kwa lengo la kuwavutia watalii wengi katika maeneo hayo.

15.6.6 Ili kuepukana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kulinda utamaduni wa Mtanzania, Serikali itasisitiza utalii wa hali ya juu wa kupangwa badala ya utalii wa holela ambao unahusisha makundi makubwa ya watalii. Itakuwa ni lazima kwa shughuli za uendelezaji/ukuzaji

#### 15.5.3 Usafiri wa Reli

Usafiri wa reli nchini unakabiliwa na matatizo makubwa ya ukosefu wa mabehewa, injini na vipuri. Kwa kuzingatia hali hiyo:

15.5.3.1 Serikali itaendeleza jitihada za kuimarisha usafiri wa reli kwa kutengeneza injini na mabehewa yaliyopo na kuagiza injini, mabehewa mengine na vipuri.

15.5.3.2 Jitihada zitaendelezwa za kushirikiana na nchi na mashirika ya kimataifa ili ziweze kusaidia juhudi za taifa katika kuimarisha usafiri wa reli nchini.

15.5.3.3 Reli ya TAZARA bado haijatumika kwa ukamilifu katika kuendeleza utalii kanda ya kusini. Juhudi zitafanywa kuhakikisha reli hii inatumika kwa ukamilifu katika kuimarisha utalii kanda ya kusini.

#### 15.5.4 Usafiri wa Majini.

Usafiri wa majini unahusu usafiri wa baharini, kwenye maziwa na mito. Matatizo yanayokabili usafiri wa majini hayatofautiani na matatizo ya sekta nzima ya usafiri. Upo upungufu mkubwa wa meli, maboti, wataalam na vipuri. Hali hii inaathiri kwa kiwango cha juu usafiri baharini, kwenye maziwa na mito. Hivyo sera italenga katika:

15.5.4.1 Kuongeza idadi ya meli na boti kulingana na uwezo wa taifa ili kukidhi mahitaji ya taifa na kukuza biashara ya utalii.

15.5.4.2 Serikali itaangalia uwezekano wa kushirikiana na nchi jirani katika kuanzisha miradi ya pamoja.

### 15.6. Uendelezaji wa Uhifadhi na Vivutio vya Utalii:

Asilimia 25 ya eneo la Tanzania limetengwa kwa ajili ya hifadhi ya wanyamapori, ndege na mazingira yao. Tamko

utalii kama ujenzi wa barabara, hoteli na huduma nyinginezo kama vile shule, hospitali na kadhalika kufanyiwa tathimini ya mazingira kabla ya utekelezaji.

**15.7 Kuimarisha Utalii wa Mikutano**

Tanzania imepata sifa nyingi katika utalii wa mikutano kutokana na kumiliki kituo maarufu cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha. Utalii wa Mikutano ni wa'ushindani mkubwa. Ili kuendeleza na kukuza utalii wa aina hii, hatuna budi kuhakikisha kwamba:

15.7.1 Huduma muhimu zitolewazo na kituo hicho zitaimarishwa ili kiweze kufikia viwango vinavyohitajika.

15.7.2 Wizara itasimamia na kuratibu kwa ukaribu zaidi shughuli za utalii wa mikutano kwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika kwa lengo la kuendeleza utalii wa aina hii.

15.7.3 Jitihada za kujenga vituo vipya vya mikutano nchini zitafanywa. Umuhimu utawekwa katika kujenga hoteli za kitalii ambazo zitakuwa pia na huduma za vituo vya mikutano vya hadhi za kimataifa.

**15.8 Kuendeleza Uwindaji wa Kitalii:**

Kutokana na utajiri mkubwa uliopo nchini, upo uwezekano mkubwa wa kuongeza kwa kiwango kikubwa pato la taifa na fedha za kigeni kutokana na uwindaji wa kitalii. Ili kuendeleza uwindaji wa kitalii:

15.8.1 Makampuni yanayofanya shughuli za uwindani wa kitalii yataimarishwa kwa kuyapatia zana za kufanyia kazi na mafunzo.

15.8.2 Hatua za kutangaza vivutio vyetu nchi za nje zitachukuliwa na utoaji huduma safi kwa watalii hao zitaendelezwa.

zo zaidi, ili kuinua kiwango chao cha utendaji kazi.

**15.10 Kuendeleza Uwekezaji wa Raslimali wa ndani na Nje:**

15.10.1 Uwekezaji wa raslimali katika sekta ya utalii utaimarishwa kutokana na umuhimu wa sekta hii katika kuchangia pato la taifa.

15.10.2 Hatua za kuzishawishi taasisi, mashirika ya umma na sekta ya binafsi ya ndani kujiingiza katika biashara ya utalii kwa kujenga hoteli za kitalii, loji, uwakala na makampuni ya usafiri zitachukuliwa.

15.10.3 Mpango huu utahusisha Jumuiya za Wananchi, Vyama Vikuu vya Ushirika, Taasisi na Mashirika ya Umma na ya Binafsi kama vile NPF, NBC, TDFL na kadhalika, Mashirika ya Dini na Watanzania binafsi wenye uwezo.

15.10.4 Ili mpango huu ufanikiwe utahitaji ushirikiano wa karibu wa Chama, Jumuiya za Wananchi, Serikali Kuu na vyombo vyake, Serikali za Mitaa na Vijiji na Vyama Vikuu vya Ushirika na vya Msingi. Aidha vikundi hivi vitashauriwa kuanzisha makampuni ya uendeshaji wa hoteli kama ilivyo kampuni ya "Hotel and Tours Management" ambayo inazo hoteli nyingi (Hotel Chains).

15.10.5 Ili kuinua kiwango cha utalii nchini, Serikali itashirikiana na Serikali, Mashirika na watu binafsi wa nje katika kuendeleza utalii nchini kwa kuanzisha miradi ya pamoja ya ubia, kuingia mikataba ya uendeshaji na kuziruhusu nchi na makampuni hayo kuanzisha miradi ya pekee.

15.10.6 Ushirikiano huu utawekewa sheria, kanuni, taratibu na mikataba ya wazi kati ya Tanzania na nchi au mashirika/watu binafsi kutoka nje zitakazohakikisha uhuru na mafanikio mengine yaliyopatikana katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii yanalindwa.

15.8.3 Serikali itaendeleza juhudi za kuvuna wanyamapori ili kukidhi mahitaji ya wananchi ya kujipatia kitoweo, matumizi mengine ya mazao yatokanayo na wanyamapori, kulinda na kuhifadhi mazingira na kuuza ziada nchi za nje. Tahadhari zitachukuliwa za kuhakikisha kwamba uvunaji huu hautahatarisha kutoweka kwa baadhi ya wanyamapori kama vile tembo, faru, chui, na wengineo.

**15.9 Kutunga au Kurekebisha Sheria Zinazohusiana na Utalii:**

Ili kuimarisha, kusimamia na kuratibu shughuli za utalii nchini, hapana budi kutunga, na kuweka sheria au kuzifanyia marekebisho zile zilizopo kwa kulingana na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyopo.

15.9.1 Serikali itazichambua na kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria muhimu zinazogusa sekta ya utalii kwa lengo la kuimarisha na kusimamia biashara ya utalii nchini kama vile Sheria ya Hoteli ya mwaka 1963, Sheria za Wakala wa Utalii ya mwaka 1969, Sheria ya Kulinda Vitega Uchumi vya Nje ya mwaka 1990, Sheria ya Hifadhi za Mbuga za Wanyama, Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro, Sheria ya Hifadhi ya Wanyama na Mimea na Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi.

15.9.2 Serikali itaimarisha sheria, kanuni na taratibu za uingizaji wa watalii, ushuru wa forodha, huduma kwa watalii, afya, usalama na kadhalika kwa nia ya kuimarisha shughuli za utalii nchini na kuzuia urasimu au usumbufu ambao watalii wamekuwa wakiupata.

15.9.3 Vyombo mbalimbali vinavyosimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusu maendeleo ya utalii vitaimarishwa kwa kupewa zana zaidi za kufanyia kazi na kuwapatia wafanyakazi wa vyombo hivyo mafun-

ajili ya maendeleo ya utalii zinapata huduma muhimu kama barabara, maji, umeme na kadhalika.

**15.11 Kuimarisha Utangazaji:**

Serikali itaunda chombo maalum cha kutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

**16. Uimarishaji wa Huduma Nyingine za Kitalii**

16.1 Ili kukabiliana na tatizo la nyumba za kulala wageni, nyumba za watu binafsi zenye hadhi na zenye usalama zitaruhusiwa kupokea na kutoa huduma za malazi na chakula kwa watalii kwa utaratibu utakaotambuliwa kisheria. Hatua za kuimarisha uhuru na usalama wa watalii wa ndani na nje zitaimarishwa ili watalii wajenge imani zaidi na taifa letu.

16.2 Katika kuimarisha utalii itahakikishwa kwamba katika maeneo ya utalii kunakuwepo huduma nyinginezo muhimu kama vile makanisa, misikiti, hospitali na shule.

16.3 Serikali itadhibiti bei za huduma za kitalii ili zisiwe kubwa sana zikaathiri biashara ya utalii.

16.4 Burdani na michezo ya aina mbalimbali hutumika kama vitegauchumi na vivutio vya utalii. Burdani hizi, licha ya kuingiza fedha za kigeni husaidia katika kutangaza utalii. Ili kuliongezea taifa pato la fedha za kigeni Serikali itaendeleza burdani zilizopo kama golf, tennis, na kadhalika na kuanzisha mpya kama vile casino na kadhalika. Aidha Serikali itahakikisha kuwa kila hoteli yenye eneo la kutosha itakuwa na mabwawa ya kuogelea na maduka madogo yanayouza bidhaa muhimu na zile za sanaa za mikono zinazoonyesha utamaduni wa Mtanzania.

16.5 Ili kuwapa motisha na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi, jitihada zitafanywa za kuhakikisha wafanyakazi wa sekta ya utalii wanapatiwa nyumba za kuishi, usafiri

15.10.7 Motisha kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wa vitega uchumi katika sekta ya utalii utakuwa ni ule uliotamkwa bayana katika Sera ya Taifa ya Uwekezaji Rasilimali ya mwaka 1990.

15.10.8 Wizara itaimarisha taratibu za uandikishaji wa vyombo vyote vya ndani na nje vinavyojihusisha na biashara ya utalii nchini, uwekaji wa viwango na utoaji motisha kwa vyombo hivyo katika uendeshaji wa shughuli zao.

15.10.9 Vivutio vya asili vilivyopo nchini ni rasilimali muhimu katika uchumi wa taifa kama vile ardhi, wanyamapori, mito, maziwa, bahari, magofu na kadhalika. Rasilimali hizi zina thamani kubwa kwa taifa. Kwa msingi huo, mikataba itakayowekwa ya ushirikiano baina ya Tanzania na nchi za nje katika biashara ya utalii itazingatia awali kwamba tayari taifa linazo rasilimali za kudumu na zenye thamani.

15.10.10. Wizara itahakikisha utaratibu mpya uliotangazwa na serikali wa kuruhusu mashirika na watu binafsi wanaouza bidhaa za Tanzania nchi za nje kumiliki sehemu ya mapato ya fedha za kigeni inatumika kwa ukamilifu katika kuendeleza sekta ya utalii.

15.10.11 Kwa zile hoteli ambazo zitakuwa na mikataba ya uendeshaji na makampuni ya nchi za nje, serikali itahakikisha kwamba:

15.10.11.1 Wataalam wa kigeni wanaongoza tu idara zile ambazo hakuna wataalam wa kizalendo wenye ujuzi na uzoefu wa kuziendesha.

15.10.11.2 Mipango kamambe ya mafunzo inafanywa ya kuwapatia mafunzo wazalendo ili waweze kushika nafasi za wataalam wa kigeni mara baada ya mikataba kumalizika.

15.10.12 Serikali itahakikisha kuwa sehemu zilizotengwa kwa

## TAMKO RASMI LA HALMASHAURI KUU YA TAIFA KUHUSU UTALII

Halmashauri Kuu ya Taifa, katika kikao chake cha kawaida kilichofanyika katika ukumbi wa Baraza la Uwakilishi Zanzibar tarehe 14 hadi 16 Februari, 1991 chini ya Mwenyekiti wake Ndugu Ali Hassan Mwinyi pamoja na mambo mengine, ilipokea na kujadili rasimu ya Sera ya Utalii iliyowasilishwa kwake na Serikali ya Muungano.

Pamoja na kuipitisha Sera hiyo, Halmashauri Kuu ya Taifa ilitoa Tamko Rasmi kuhusu nafasi ya umuhimu wa utalii katika kuimarisha uchumi wa Taifa, kama ifuatavyo:

1. Kwa muda mrefu sasa, nchi yetu ilikuwa haijatumia kikamilifu utajiri mkubwa wa maliasili tuliyo nayo, na vivutio vingine vya kitalii vilivyopo, katika kuinua uchumi wetu. Hii imetokana na kutokuipa uzito wa kutosha nafasi kubwa iliyonayo sekta ya utalii katika maendeleo ya taifa.
2. Halmashauri Kuu ya Taifa imeridhika kwamba kuwapo kwa Sera ya Utalii ni hatua muhimu ya mwanzo. Kwani Sera inatoa ufafanuzi dhahiri wa azma na mwelekeo wa Chama na Serikali kuhusu suala zima la maendeleo ya Utalii katika kipindi kilichopo. Sera hiyo inalenga katika kuikuza na kuimarisha sekta ya utalii ili uwezo wake mkubwa utumike kwa ukamilifu katika kuchangia mapato ya taifa kwa jumla, na hasa mapato ya fedha za kigeni; kuongeza ajira ya wananchi; na kuchangia katika kupanua uzalishaji bidhaa na utoaji huduma mbalimbali zinazohitajiwa na sekta hii.
3. Kwa hiyo kuanzia sasa, Halmashauri Kuu ya Taifa inaelekeza kwamba jitihada kubwa zaidi za Serikali, za vyombo vya uchumi vya ndani na nje ya nchi, na za wawekezaji

unaoaminika wa kwenda kazini na maslahi mengineyo ili kuongeza ari na kuinua viwango vya utendaji kazi.

16.6 Mkazo maalum utawekwa katika kuinua kiwango cha utoaji huduma katika hoteli za kitalii ili vilingane na viwango vya kimataifa.

**17. Mengineyo:**

17.1 Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania itaimarisha ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza utalii nchini.

17.2 Wizara kwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika itahakikisha kuwa hatua zinachukuliwa mara moja kuyatatua yale matatizo ambayo yamo ndani ya uwezo wetu. Uzembe, ubadhirifu, udanganyifu, ufujaji wa mali ya umma, wizi na hujuma mbalimbali vitapigwa vita.

17.3 Wizara itaweka malengo ya uzalishaji katika sekta nzima ya utalii na kuhakikisha malengo hayo yanatekelezwa. Kwa upande wa sekta ya umma wafanyakazi watafikiriwa kupewa bonasi kama motisha endapo malengo yatafikiwa.

**Mwisho:**

18. Sekta ya Utalii ni sekta inayotegemewa sana katika kuchangia kuinua pato la taifa iwapo itaendelezwa hasa ikizingatiwa utajiri mkubwa wa vivutio uliopo. Kwa msingi huo utekelezaji wa Sera ya Utalii utahitaji kukusanya nguvu zote ili kuweza kuzalisha matunda yaliyotarajiwa. Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira ndiyo yenye jukumu kubwa la kuhakikisha Sera hii inatekelezwa kwa kuandaa programu nzuri ya utekelezaji na kuisimamia.

19. Kutokana na uhusiano mkubwa uliopo kati ya sekta ya utalii na sekta nyingine za uchumi, upo ulazima mkubwa wa Serikali na vyombo vyake kushirikiana katika kutekeleza Sera hii.

## VIVUTIO KWA WANAOWEKA RASLIMALI ZAO TANZANIA

*(Imenukuliwa kutoka kwenye Sera ya Taifa ya Uwekezaji wa Raslimali)*

Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vivutio vizuri ili kuwahimiza wawekezaji wa raslimali wa humu nchini na nje kuweka raslimali zao Tanzania. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Sera hii, vivutio vifuatavyo vitakuwepo. Vivutio hivi vitawafaidia wawekezaji raslimali ambao wamepata hati ya kukubaliwa inayotolewa na Kituo cha kuendeleza uwekezaji wa Raslimali (Investiment Promotion Centre - IPC) kufuatana na masharti yaliyowekwa na Sera hii na kwa mujibu wa miongozo ya utekelezaji itakayowekwa na IPC.

**Vivutio vya Kodi:**

Kutakuwa na msamaha wa kodi wa muda maalum wa miaka mitano ya mwanzo ya uzalishaji ambako kodi haitatozwa kwenye faida. Baada ya hapo, kodi itatozwa kama ifuatavyo:

- Asilimia 50 ya faida inayotozwa kodi kwa miradi ambayo siyo ya wakazi.
- Asilimia 45 ya faida inayotozwa kodi kwa miradi ambayo ni ya wakazi.
- Sheria za kodi zitatumika kuainisha wakazi na wasio wakazi.

Vivutio hivyo vitatolewa wakati wa upanuzi, ubadilishaji wa uzalishaji au biashara na ukarabati kama itakavyoidhinishwa na IPC.

raslimali binafsi, zielekezwe katika kuendeleza sekta ya utalii, ili iweze kutoa mchango wake kwa ukamilifu.

Halmashauri Kuu ya Taifa inawakumbusha washiriki wote kwamba wanaweza kutumia fursa ya vivutio na motisha zilizotolewa na Sera mpya ya Uwekezaji Raslimali nchini (The National Investment Promotion Policy). Aidha, viongozi wa Chama na Serikali katika ngazi zote, na vyombo vyote ambavyo huduma zake zinahusika na utalii kwa namna moja au nyingine, zitoe ushirikiano wao wa dhati katika kusaidia kufanikisha maendeleo ya sekta hii ya utalii."

vivutio kwa tekinolojia ya humuhumu nchini utawekwa.

**Riba:**

Kwa kutambua jitihada za kimataifa zinazoendelea hivi sasa za kupunguza mzigo wa madeni na ulipaji wa fedha nje, Serikali inahimiza uwekezaji ambao sio wa mikopo. Kwa hiyo, ili kupunguza madeni ya nje, viwango vya kodi itakayotozwa kwenye riba inayolipwa kwa mikopo ya nje itabakia kuwa asilimia 20.

**Kodi kwa Mishahara ya Wataalamu wa Kigeni:**

Serikali inatambua mchango unaotolewa na wataalamu wa kigeni na inaweka umuhimu katika haja ya kuwaajiri wataalamu wa kigeni wenye ujuzi na utaalamu unaotakiwa. Wataalamu hawa wa kigeni wanahitajika ili kuwafunza wataalamu wa Kitanzania na kuongeza wafanyakazi wenye ujuzi katika maeneo muhimu. Pamoja na kiwango cha juu cha kodi ya binafsi inayotozwa kuwa asilimia 50, Serikali pia inatoa nafuu ya kodi kwa wataalamu wa kigeni chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato namba 112 ya mwaka 1976.

**Kodi zisizodhihirika (indirect taxation):**

Kodi zisizodhihirika nchini Tanzania ni pamoja na kodi ya forodha, kodi ya mauzo na ushuru wa "excise". Kodi hizi zinazotozwa bidhaa zinazoingizwa nchini zinafanana na zile zinazotozwa na nchi nyingine zinazoendelea na kwa ujumla hazitazidi asilimia 60 kwa kila kitu tofauti kinachoingizwa nchini na wawekezaji wa raslimali. Hata hivyo, ili kuhimiza raslimali katika maeneo yanayopewa kipaumbele, Serikali imeweka vipengele kadhaa ambavyo vinaondoa kabisa kodi ya forodha, kodi ya mauzo na ushuru wa "excise".

**Vivutio vya Fedha za Kigeni:**

Serikali itapanua vivutio vilivyopo ambavyo ni pamoja na:

– Kuendeleza mpango ambao wanaouza bidhaa nje

**Kodi kwa Vyama vya Ushirika:**

Vivutio pia vitatolewa kwa Vyama vya Ushirika ambavyo vimeandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1982 na ambavyo vinakuwa na raslimali zao. Vyama hivi vitakuwa na haki ya kupata msamaha wa kodi ambako, kwa muda maalum, kodi haitatozwa kwa faida wanazopata kama ilivyo kwa wawekezaji raslimali wengine. Hata hivyo, baada ya muda huo, viwango vya kodi itakayotozwa kwa miradi yao iliyoidhinishwa kitakuwa asilimia 22.5.

**Kodi kwa Mapato Binafsi:**

Muwekezaji raslimali pekee ambaye miradi yake imeidhinishwa na IPC pia atafaidika na msamaha wa kodi kwa muda maalum wa miaka mitano ya kwanza ya uzalishaji. Hata hivyo, viwango vya kodi vitakavyotumika baada ya kipindi hiki cha mwanzo cha miaka mitano vitabakia kama vilivyoelezewa katika Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 ambayo inaelezea utozaji, ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi ya mapato.

**Mgawio (Dividends):**

Kiwango cha sasa cha asilimia 20 kwa wasio wakazi na asilimia 10 kwa wakazi kitapunguzwa kufikia asilimia kumi (10) kwa wasio wakazi na asilimia 5 kwa wakazi. Mgawanyo utatolewa kulingana na Sheria ya Makampuni namba 22 ya mwaka 1972, kipengele kinachohusiana na urekebishaji wa mgawanyo na ziada na masuala mengineyo. Chini ya Sheria hii inaainisha utaratibu wa ugawaji wa faida na matumizi ya mapato ya baadhi ya Bodi na Mashirika na inaweka vipengele vinavyohusu makampuni.

**Mirabaha (Royalties):**

Ili kuhimiza ubunifu na upatikanaji teknolojia sahihi, viwango vya kodi inayotozwa kwa mirabaha ya teknolojia inayoingizwa nchini vitapunguzwa kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 20 kwa jumla ya kiasi kinacholipwa. Utaratibu wa

mbili:

- — Malimbikizo ya malipo ya nje yanayotokana na mikataba inayohusu madeni;
- — Malimbikizo ya malipo ya nje yanayotokana na masuala yanayohusiana na madeni, lakini ambayo hayana mikataba yoyote ya awali inayohusu madeni.

**Kupeleka Fedha Nje:**

Serikali inayatambua matatizo ya fedha za kigeni yanayokabili uchumi wa Tanzania. Hata hivyo, Serikali pia inatambua kwamba wawekezaji wa raslimali wanahitaji uwezo wa kuaminika wa kuweza kupeleka fedha nje kwa ajili ya matumizi yanayohusiana na miradi yao. Kwa kuzingatia haya, utaratibu wa kuweka nje kiasi fulani cha fedha zinazopatikana kutokana na kuuza bidhaa na huduma nje utapanuliwa ili kuwawezesha wote walioko chini ya utaratibu huu kutumia kiasi kinachofikia asilimia 50 ya mapato ya fedha za kigeni kufanya malipo nje.*

Pamoja na utaratibu huu wa kuchukua kiwango kilichowekwa cha mapato ya fedha za kigeni, hatua nyingine ambazo zinatoa kipaumbele katika matumizi mazuri ya fedha za kigeni, zitahusu maeneo yafuatayo:

- — Njia za malipo kwa Tanzania na kutoka Tanzania;
- — Kutoa, kuhamisha na kukubali dhamana kwa ajili ya malipo yanayowahusu wakazi na wasio wakazi;
- — Malipo kwa bidhaa zinazoagizwa nje;
- — Ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni pamoja na uwekaji wa fedha katika akauti za nje;
- — Utaratibu wa wakazi kupata, kumiliki na kutumia mali za nje;

---

* *Kiwango hiki kimerekebishwa.*

wanaruhusiwa kuchukua sehemu ya mapato yao katika fedha za kigeni ili waweze kuagizia bidhaa ambazo wanazihitaji kwa shughuli zao.


- Upendeleo katika ugawaji wa fedha za kigeni kwa watengenezaji wa vitu vinavyouzwa nje au vile ambavyo vinapunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje.
- Kulipa madeni ya muda mrefu na magawio kwa kutumia fedha ambazo wauzaji wa bidhaa nchi za nje wanaruhusiwa kuwa nazo nje.

Wakati juhudi kubwa zitafanyika kuhakikisha kwamba wawekezaji raslimali wanapata fedha za kigeni kwa haraka, hata hivyo fedha hizo za kigeni zitatolewa kutegemeana na:

- Jumla ya fedha halisi za kigeni zitakazozalishwa na mradi;
- Uokoaji mkubwa na wa dhahiri unaotokana na mradi;
- Kiwango cha upatikanaji wa tekinolojia;
- Nafasi za kazi ambazo mradi utatoa;
- Jinsi gani watu wa humu humu nchini wataajiriwa katika mradi na
- Mchango wa jumla wa shughuli hiyo katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

**Malimbikizo ya Malipo ya Nje:**

Ili kuharakisha uwekezaji wa raslimali kutoka nje, Serikali imeweka utaratibu ambao malimbikizo ya malipo kutoka nje yatatumika kwa kuwekeza raslimali katika miradi iliyoidhinishwa. Malimbikizo ya malipo ya nje ambayo yatatumika kama raslimali itahesabiwa kama raslimali kutoka nje. Utaratibu huu unaruhusu baadhi ya fedha hizi kutumika humu nchini katika maeneo yaliyoidhinishwa ambayo yanatoa mchango mkubwa kwa uchumi. Malimbikizo haya ni ya aina



VIVUTIO MUHIMU VYA UTALII TANZANIA
UGANDA
KENYA
RWANDA
BURUNDI
ZAIRE
ZAMBIA
MALAWI
MOZAMBIQUE
T A N Z A N I A
KEY
SCALE 1:6,000,000
REFERENCE

— Ajira ya wataalamu kutoka nje;

— Mikopo wanayopata na wanayoitoa wasio wakazi.

**Vyanzo vitakuwa ni pamoja na:**

— Fedha za kigeni ambazo nchi inazipata kutokana na uuzaji nje wa bidhaa na huduma;

— Mikopo na misaada kutoka nje;

— Mikataba ya biashara ya kubadilishana bidhaa;

— Fedha zinazotokana na utaratibu wa wauzaji bidhaa na watoaji huduma nje ya Tanzania kubakiza kiasi cha fedha za kigeni nje.

— Mikopo inayotolewa na wenye bidhaa nchi za nje.

ANNUAL GENDER STUDIES CONFERENCE (AGSC '96)

# SITUATION OF THE PRIMARY SCHOOL WOMEN TEACHERS DURING THE ECONOMIC CRISIS IN TANZANIA

*Bibiana Shauri Komunte*

Paper Presented to AGSC '96, December 5th - 8th
IFM, Dar es Salaam.

# SITUATION OF THE PRIMARY SCHOOL WOMEN TEACHERS DURING THE ECONOMIC CRISIS IN TANZANIA

By: Bibiana Shauri Komunte
(Dip Ed.; B.A. (Hons); M.A.)
SECONDARY SCHOOL TEACHER AND PART-TIME LECTURER

P.O. Box 36,
MZUMBE
TANZANIA

## 1.0 INTRODUCTION

### 1.1 TEACHERS POPULATION:

According to the basic statistics in Education (June, 1996) there are 105,280 primary school teachers in Tanzania. Out of these 45,482 (43.2%) are men and 59,798 (56.8%) are women. This means that teaching is one of the wage employment jobs in which the number of women is almost the same as the men. Nevertheless, women are more than men. Tanzania cannot therefore ignore the women teachers in development.

### 1.2 THE ECONOMY:

Tanzania's economy is based on small holder agricultural producers. This sector employs about 90% of the country's labour force and contributes 45% of the Gross Domestic Product (GDP) 20% of the country's labour force are employed. Teachers are among the employed workers. However, it should be barn in mind that Tanzania workers are also engaged in small scale agriculture and livestock keeping to subsidise their salaries.

### 1.3 THE ECONOMIC CRISIS IN TANZANIA:

The Economic Crisis in Tanzania is historical. The decline of the economy can best be analysed within five phases. First phase was 1961-67 when reliance on private enterprises, tolerance of foreign investment and stress on the objectives of growth in per capita income dominated.

The second phase was 1967-1976 when socialism and self-reliance with rural and agricultural development were key areas of the policy action. The economy had performed relatively well up to the mid 1970s with annual growth rate above 5%.

The third phase was 1976-1984 when there was a general decline in agricultural production coupled with an under utilisation of the available industrial capacity. This was the most crisis ridden phase. The GDP growth rate fell to an average of 2.6% during 1978-1981. There was emergency of pseudo-merchant class. Hoarding and racketeering dominated the economy. This was also the period when the state opted for allocating a larger share of the available resources to the more directly productive sectors of the economy than to the social service sector.

The fourth phase was 1985-1989 when difficult economic conditions were elaborated in the 1984/85 budget. This was followed by policies falling under the Economy Recovery Programme (ERP). Emphasis was placed on directly productive sector leaving the social services such as education and health intact, but dry. In this phase, therefore, the primary school teachers' respect which they were receiving from the public in general and from government leaders in particular started to deteriorate. This was because teachers' input and output is normally intangible and what they render is social service which was ignored by the government in the fourth phase.

In the fifth phase, that is, 1990 to-date the government has opted for a strategy of correcting the negative social consequences of ERP. This is the underlying spirit of the Economic and Social Adjustment Programme (ESAP) which states that the government will not be in a position to restore the social services to levels achieved in the 1970s but it will try its best to improve the social services. Formation of workers' unions such as the Tanzania Teachers Union (TTU) is one of the measures. At least through the TTU primary school teachers will speak out their grievances. Eventually these teachers will restore their old respect as well as be in a better position to alleviate their poverty.

## 2.0 THE ROLE OF WOMEN TEACHERS IN THE SOCIO-ECONOMIC DEVELOPMENT IN TANZANIA

Population statistics show that 53% of the Tanzania population is made up of women. This means that the development of this nation cannot ignore the contribution of the largest group. It is the woman who dominate in the backbone of the economy, that is, agriculture. 87.8 % of the womenfolk are engaged in one way or another in agricultural product.

Women teachers are also engaged in one way or another in agricultural activities and other income generating activities such as selling of food stuffs, tuition, shops etc, in order to alleviate the difficulties of the Tanzanian poverty ridden economy.

It should be born in mind that besides income generating activities teachers also have other roles. Teaching more than twenty periods per week and other school extra curriculum activities capture much of teachers' time.

Women teachers have other traditional roles at their homes. These include child care, husband care, care of relatives and sick persons. Due to all these responsibilities women teachers tend to be double disadvantaged in the Tanzania society. The possibilities for primary school women teachers in Tanzania to-day to improve themselves professionally or to enter into managerial positions or big business career are certainly far from being viewed. Both women and men teachers are given equal opportunities for education, cultural and professional advancement. Nevertheless, men teachers, in spite of cultural reasons and gender relations are in a better position to develop themselves than women teachers.

## 3.0 THE WOMEN TEACHERS' CONTRIBUTION AND PARTICIPATION IN ECONOMIC DEVELOPMENT: A CASE STUDY OF MZUMBE WARD

Mzumbe Ward is in Morogoro (Rural) District in Morogoro Region, Tanzania. According to government statistics of July, 1996 Mzumbe Ward has 85 primary school teachers among whom 32 are men and 53 are women.

Women teachers in Mzumbe Ward, just like other women teachers in Tanzania are aware of their personalities, the Tanzania's economic crisis, their socio-economic constraints and their position as women and as teachers. They have encouraged each other to undertake various income generating activities in order to improve their economic status. In this section we are going to discuss experiences of the Mzumbe Ward Women teachers' participation in economic development.

### 3.1 THE WOMEN TEACHERS' SITUATION:

Research findings have shown that the Mzumbe ward women teachers are very busy. Among the 50 women teachers interviewed 45 (90%) women teachers have got 20-30 periods per week. It was also found out that 25 (50%) women teachers stayed far from their schools therefore they spent a lot of time walking to and from schools.

It was also found out that 30 (60%) Women are grade III C hence they receive less than T.shs. 28,000/= per month. Inspite of receiving such a meagre salary 30 (60%) of the teachers take care of three and/or above children and other relatives. Therefore all the women teachers (100%) are engaged in economic activities which, due to lack of time generate an average of T.shs.200/= only per day.

### 3.2 CONSTRAINTS WHICH WOMEN TEACHERS FACE:

#### 3.2.1 Lack of Teachers' Houses:

There are no teachers' houses at the school campuses. Therefore teachers rent rooms far from the school. Sometimes they are obliged to pay bus fare to travel to and from school. This problem is well known but nothing is done to improve the situation. The journey to and from school for five days in a week hampers the teachers' economic development in that the teachers waste a lot of time on the way.

#### 3.2.2 Lack of Capital:

The primary school women teachers income is extreamly small. They are therefore too inadequate to start a big economic enterprise. The women teachers in Mzumbe Ward are ot given any house or transport allowances.

#### 3.2.3 Lack of Information:

The primary school women teachers do not get valuable information concerning their businesses, markets, technology etc. Besides, they are not access to the donor organisations which could provide loans and/or assistance to them. Therefore they lack financial support. Among the 50 women teachers interviewed 60% are engaged in selling food stuffs like burns and ice cream, selling goods from their gardens and tuition classes. However, they receive about T.shs.200/= only per day. The other 40% remaining do not have any project because they do not see any gain from them.

#### 3.2.4 Lack of time:

Due to the combined roles as mothers, teachers (workers) and business women there is no time for better future plans looking after their economic activities, school activities and participate in other social activities.

From the above constraints, we need to understand the constraints that are faced by women in different fields in which they participate so that deliberate efforts are made to remove these constraints.

## 4.0 THE ECONOMIC CRISIS, WOMEN TEACHERS IN DEVELOPMENT AND THE WAY FORWARD

Tanzania appears to be still politically stable. A lively debate about the future course of Tanzanian's political development has culminated into the adoption of a multi-party democracy. It is not yet known what the drive to political liberalism implies in economic terms. There is more likelihood that an element of continuity with the past and/or present will be preserved in the economic sphere. In any case, addressing past economic mistake is likely to be done in possible policy shifts in the context of the on going economic recovery.

With the emerging teachers' union, women teachers' constraints will be more pronounceable with a consequence of their educational, social and economic development. The future of women teachers in development will depend on the recognition of their importance by the government.

## 5.0 CONCLUSION:

It is undeniable that eduction is the bedseed of the development of any country. It is no doubt that teachers are important people due to their contribution in education in the country. There is no question that increasing burden of the country's poverty falls most heavily upon women, women teachers being among them. Poverty cannot be eradicated without the contribution of women in general and women teachers in particular.

Therefore excluding women teachers from development not only leaves the situation worse but also impoverishes the whole society.

## REFERENCES:

1. Bank of Tanzania (1992) "Economic Performance Annual Report 1991/92". Dar es Salaam.

2. Bureau of Statistics (1988) "1988 Population Census: Preliminary Report" Dar es Salaam: Mimeo

3. Bureau of Statistics and Ministry of Community Development Women Affairs and Children (1995) Analysis of African Women and Men: The Tanzania Case. Dar es Salaam: MCDWAC

4. Maliyamkono, T.L. and M.S.D. Bagachwa (1990) The Second Economy In Tanzania. Athens: Ohio University Press and James Currey.

5. Meikle, S. (1993) Structural Adjustment Terminologies and Issues for Debate UCL.

6. Ministry of Community Development Women Affairs and Children (1992) Policy on Women and Development in Tanzania , Dar es Salaam: MCDWAC

7. Ministry of Education and Culture (1996) 'Basic Statistics in Eduction 1991-1995" Dar es Salaam: National Data.

8. Mwaga, J. (1996) Professional Staff Development in Tanzania Education System: Theory and Practice. Dar es Salaam: Mture Publishers.

9. Wagao, J.H. (1993) "Tanzania Economy: Retrospect and Prospects in change". No.1